

HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

SHULE YA SEKONDARI KARITU,

S. L. P 31,

TAREHE: 01/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KARITU ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2019

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Karitu mwaka **2021**

Muhula wa kwanza wa masomo unanza tarehe **11.01.2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15.01.2021** (ndani ya siku saba) baada ya hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule

a) Sare ya shule kwa wavulana

- (i) Suruali ya kijani kitambaa kizito namba moja (01) (ziwe mbili)
- (ii) Shati jeupe mikono mifupi (ziwe mbili)
- (iii) Tai ndefu ya kijani (kitambaa cha suruali) isiwe ya lastiki
- (iv) Mkanda wa ngozi (mweusi)
- (v) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba
- (vi) Soksi nyeupe (jozi mbili)
- (vii) Sweta la kijani kibichi.
- (viii) Tisheti rangi ya blue bahari

MUHIMU: Suruali ya shule isiwe modo (isiwe ya kubana na iwekwe marinda mawili kila upande)

Sare ya michezo

- (i) Tisheti mbili (02) rangi nyekundu na rangi ya zambarau.
- (ii) Kaptula (bukta) mbili (02) rangi nyeusi na rangi nyekundu
- (iii) Raba za michezo na soksi za michezo (ndefu)

b) Sare ya shule kwa wasichana

- (i) Sketi ya kijani kitambaa kizito namba moja (01) (ziwe mbili).
- (ii) Shati jeupe mikono mifupi (ziwe mbili)
- (iii) Tai ndefu ya kijani (kitambaa cha sketi) isiwe ya lastiki.
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba
- (v) Soksi nyeupe (jozi mbili)
- (vi) Sweta la kijani kibichi.
- (vii) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule

MUHIMU: Sketi ya shule iwe ya marinda na iwe ndefu kupita magoti

Sare ya michezo

- (i) Tisheti mbili (02) rangi nyekundu na rangi ya zambarau
- (ii) Sketi ya michezo (rangi - damu ya mzee) pamoja na suruali - traki
- (iii) Raba za michezo na soksi za michezo

2.2. Vifaa vya taaluma: Counter book (kaunta buku) Q3 (ziwe 09) daftari ndogo za kawaida nne (04), kalamu za kutosha za wino wa bluu na nyeusi mkebe wa hesabu

3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini katika shughuli za jioni (baada ya masomo)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i) Kutunza mali za umma

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa/kusimamishwa shule

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
- i) Kuoja/ kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni. Mwanafunzi hatapokelewa iwapo hatokuja na Form hii ikiwa imekamilika.
- (b) Ni lazima mwanafunzi aletwe na mzazi/mlezi siku ya kuripoti shuleni, tofauti na hapo mwanafunzi hatapokelewa

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

6.0. Kumbuka kumpatia mtoto elimu ni lazima, hivyo mtoto akishindwa kuripoti kwa wakati hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi atakayeshindwa kuleta mtoto wake kwa wakati shuleni.

KARIBUNI SANA KARITU SEKONDARI

.....
MASHAURI M. BATURE
MKUU WA SHULE
0715 898 880